Msaada Kutoka Upande Mtakatifu

na

Ellis P. Forsman

(Help From The Divine Side)

Msaada Kutoka Upande Mtakatifu

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 12, 2011

Msaada Kutoka Upande Mtakatifu

Zaburi 46: 1-11

Zab. 46:1-3, 7, "*Mungu kwetu sisi ni kimbilio na nguvu, msaada utakaonekana tele wakati wa mateso. Kwa hiyo hatutaogopa ijapobadilika nchi, ijaapotetemeka milima moyoni mwa bahari. Maji yake yanapovuma na kuumuka, ijapopepesuka milima kwa kiburi chake. BWANA wa majeshi yu pamoja nasi, Mungu wa Yakobo ni ngome yetu.*"

Watu wengi wanaonekana kuhitimisha kwamba Mungu yuko mbali na majukumu mengi akiendesha anga asiweze kuwajali; na kwamba Yesu tayari ameshafanya yote anaayopaswa kufanya; na kwamba malaika hawawezi kufanya chochote, kwao. Hii inawaongoza katika kutegemea ubinafsi wao uliodhaifu wanapohitaji msaada toka kwa Mungu. Hii inapatikana ikiwa tu wataitumia.

Mtunzi wa Zaburi Daudi alitambua msaada ambao Mungu anawapa wale wampendao.

Zab.121:1-3, "*Nitayainua macho yangu niitazame milima, msaada wangu utatoka wapi? Msaada wangu u katika BWANA, aliyezifanya mbingu na nchi. Asiuache mguu wako usogezwe; asisinzie akulindaye;*"

Ili Mungu asaidie watu wake itakuwa ni kazi rahisi kwa aliyetengeneza na kuumba ulimwengu wote.

- Mungu aligawanyisha bahari ya shamu.
- Yesu alizaliwa na bikra.
- Yesu na mitume waliwafufuaa watu toka kwa wafu.
- Yesu alifufuka toka kwa wafu aliposulubishwa.
- Machache kati ya mifano mingi ya msaada unaotoka upande Mtakatifu.

Msaada mtakatifu nyakati za majaribu.

Jambo moja ambalo limempiga mwanadamu toka wakati wa mwanzo ni jinsi ya kushughulikia majaribu mengi yaliyopo mbele yake. Sio kila mmoja anajaribu linalofaanana na la mwenzake. Shetani anajua madhaifu ya kila mmoja na anaweka jitihada zake katika sehemu hizo.

Hataivyo, majaribu haya ni kawaida kwa mwanadamu. Kuna 1 Kor. 10:13, "*Jaribu haalikuwapata ninyi isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili.*"

Je tumeachwa ili tujikinge wenyewe dhidi ya Shetani katika kushughulikia majaribu haya? Hapana. Mungu ameshahaidi atatusaidia.

Kwanza, ameahidi kwamba hatatuacha tujaribiwe kuliko tunavyoweza. Kama tukisema kwamba majaribu yaliyoko mbelke yetu ni vigumu kubeba, basi tunamfanya Mungu kuwa mwongo na hutuacha tuingie kwenye tamaa zetu kirahisi.

2 Pet. 2:9, "*Basi Bwana ajua kuwaokoa watauwa na majaribu na kuwaweka wasio haki katika hali ya adhabu hata siku ya hukumu.*"

Mungu anaruhusu tujaribiwe kwa sababu anajua kwamba tukishinda majaribu yetu kwamba tutakuwa watu bora.

Yakobo 1:2-3, "*Ndugu zangu hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi.*"

Pili, ameahidi kwamba tunapojaribiwa kuna njia ya kutokea. Itafute! Iko pale. Ameahidi.

Unapoanza kuweka uwiano wewe binafsi pamoja na sababu zilizotolewa katika majaribu yako kwamba unajitoa kwa Shetani. Fikiria, Yesu atasema nini. Yesu atafanya nini?

Yesu alishinda majaribu kama hayahaya tunayokumbana. Je alilishughulikiaje?

- Mat. 4:1-11, "*Kisha Yesu alipandishwa na Roho nyikani, ili ajaribiwe na Ibilisi. Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa. Mjaribu akamjia akamwambia, ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mikate. Naye akajibu akasema imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu. Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini kwa maana imeandikwa, atakuagizia malaika zake; na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mgu wako katika jiwe. Yesu akamwambia tena imeandikwa usimjaribu Bwana Mungu wako. Kisha ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu na fahari yake; akamwambia haya yote nitakupa ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia, nenda zako Shetani; kwa maana imeandikwa Msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake. Kisha Ibilisi akamwachaa; na tazama wakaja malaika wakamtumikia.*"
- Heb. 4: 15, "*Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi.*"
- Heb. 2:18, "*Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.*"

Kwa sababu Yesu alipitia majaribu haya yote kwa mafanikio, anafahamu jinsi ya kutuokoa kutokana na majaribu.

Msaada mtakatifu kila wakati wa hitaji.

Tunaweza kupokea msaada mtakatifu siyo tu tunapojaribiwa, bali hata wakati wa hitaji au shida.

Heb. 4:14-16, "*Basi ikiwa tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye aliyejaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujaasiri ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"

Mara nyingi tukiwa katikati ya dimbwi la matatizo, tunamsahau Mungu na kujaribu kushughulikia matatizo hayo wenyewe. Wasiwasi wetu huwa juu; tunakuwa na mashaka na hatuwezi kulala usiku; tunajikuta tunalumbana na wenza wetu pamoja na watoto. Yote ni kwa sababu tunajaribu kusuhisha matatizo yetu binafsi.

Paulo alipata neema ya kumsaidia wakati wa mahitaji.

2 Kor. 12:1-9, "*Sina budi kujisifu ijapokuwa haipendezi; lakini nitafikilia maono na mafunuo ya Bwana. Namjua mtu mmoja katika Kristo yapata sasa miaka kumi na mine, (kwamba alikuwa katika mwili sijui; kwamba alikuwa nje ya mwili sijui; Mungu anajua). Mtu huyo alinyakuliwa juu mpaka mbingu ya tatu. Nami namjua mtu huyo, (kwamba alikuwa katika mwili sijui; kwamba alikuwa nje ya mwili sijui; Mungu anajua); ya kuwa alinyakuliwa mpaka Peponi, akasikia maneno yasiyotamkika, ambayo haijuzu mwanadamu ayanene. Kwa habari za mtu kama huyo nitajisifu; lakini kwa ajili ya nafsi yangu sitajisifu, isipokuwa kwa habari ya udhaifu wangu. Maana kama ningetaka kujisifu singekuwa mpumbavu, kwa sababu nitasema kweli. Lakini najizuia ili mtu asinihesabie zaidi ya hayo ayaonayo kwangu au kuyasikia kwangu. Na makusudi nisipate kujivuna kupita kiasi, kwa wingi wa mafunuo hayo nalipewa mwiba katika mwili, mjumbe wa shetani ili anipige, nisije nikajivuna kupita kiasi. Kwa ajili ya kitu hicho nalimsihi Bwana mara tatu kwamba kinitoke. Naye akaniambia, Neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu. Basi nitajisifia udhaifu wangu kwa furaha nyingi, ili uweza wa Kristo ukae juu yangu.*"

Wasomi wengi wanaamini katika udhaifu wake ungetazamwa kwa jicho baya. Mara tatu Paulo aliomba kwamba udhaifu wake uondolewe kwake, lakini Mungu akasema, "*Neema yangu yakutosha, maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu.*" Paulo alikubaliana hili; na hakulaumu. Kama udhaifu ungekuwa umfanye kuwa na nguvu, basi akasema, "*Nitafurahi ndani yake.*"

2 Tim. 3:10-17, "*Basi wewe umeyafuata mafundisho yangu, na imani na uvumilivu, na upendo, na saburi; tena na adha zangu na mateso, mambo yaliyonipata katika Antiokiaa, katika Ikonio, na katika Listra, kila namna ya adha niliyoistahimili, naye Bwana aliniokoa katika hayo yote. Naam, na wote wapendao kuishi maisha ya utauwa katika Kristo Yesu wataudhiwa. Lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendelea, na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika. Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na*

kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao; nay a kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo Yesu. Kila andiko yenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."

Paulo alitaja mara nyingi mambo tofauti yaaliyomtokea akiwa katika huduma ya Kristo. Leo, wengi wanaweza kujiuzulu na kusema kwamba Mungu yu kinyume na wao anaporuhusu mambo haya yawatokee. Paulo alisemaa yalimfanya kuwa na nguvu na akajifunza upole kutokana na mambo hayo. Hakuwahi kujiuzulu kwa Mungu.

Kama kweli tuna haki na tunapoliombea jambo fulani na halitokei haimanishi kwamba Mungu ametugeuzia mgongo. Kwa usahihi anaweza kuwa na sababu zake ya kutotuhakikishia kile tunachokitarajia; au aanaweza kuileta kwa njia nyingine au nyakati zingine kuliko tunaavyoweza kudhani. Nikitazama nyuma katika maisha yangu, naweza kuuona mkono wa Mungu ukifanya kazi katika kubadilisha hayo, kwa wakati yanapotokea, sikuweza kuelewa na sikuweza pia kuona. Hivyo, tunapaswa kufaanya kama Paulo na kuyakubali mambo haya yanapotokea na usilalamike au usiwe mtu asiye na subira. Yesu hakuwahi kuwa na mto wa kuegesha kichwa chake.

Usijingize sana katika kushughulikia mambo katika maisha haya.

Ahadi za Mungu ni nyingi kwa wale wamfuatao katika mambo ya kiroho kuliko mambo ya muda mfupi.

Heb.13:5-6, " *Msiwe na tabia ya kupenda fedha; mwe radhi na vitu mlivyo navyo; kwa kuwa yeye mwenyewe amesema, sitaakupungukia kabisa, wala sitakuacha kabisa. Hata twathubutu kusema Bwana ndiye anisaidiaye, sitaogopa; mwanadamu atanitenda nini?*"

Ni jambo la asili kwa mwanadamu kufikira mambo yanayomhusu, lakini Mungu hataki tuwe hivi.

Kuwa na maisha yaliyojawa maombi pamoja na Mungu. Kuwa karibu naye naye atakuwa karibu yako na kukusaidia kama kweli unamhitaji.

- Heb. 4:16, "*Basin a tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kutapata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"
- "*…anajibu tunapohitaji msaada wake.*" (Kasi njema.)
- Fil. 4:6-7, "*Msijisumbue kwa neno lolote; baali katika kilaa neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru haja zenu na zijulikane na Mungu. Na imani ya Mungu ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu.*"

Mungu aanafahamu mahitaji yetu, laakini bado anahitaji maombi yetu yamfikie kwa ajili ya kushughulikia matatizo haya. kwa kufanya haya ameahidi imani ili kutunza mioyo na akili

zetu. Kulala usiku ni rahisi zaidi ni rahisi sana kwamba wanaomfahamu Mungu wako kwenye matatizo.

Na pia ni rahisi sana kuzifanyia kazi hayo matatizo tukijua kwamba Mungu yu pamoja nasi.

Fil. 4:13, "*Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye ndugu.*"

Muwekee matatizo yako.

1 Pet.5:7, "*Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.*"

Kwa mukhtasari hii inamanisha kumpa Mungu vyote, na kukaa na kutofanya chochote. Hiki sicho ambacho Mungu alikusudia. Anatutaka kufanya jambo na alafu atatusaidia. Kwa mfano:

Tunafahamu kwamba hatupaswi kuyajali haya ya muda mfupi, isipokuwa mambo ya kiroho. Je hii inamanisha kwamba tusifanye kazi?

1 Tim.5:8, "*Mtu asiyewatunza wa kwake, hasa wale wa nyumbani kwake, ameikana imani, na mbaya kuliko asiyeamini.*"

- Efe. 4:28, "*Mwizi na asiibe tena, bali afadhali afanye kazi, akifanya kazi kwa mikono yake kwa mambo mema, ili aweze kupata kitu chaa kumpa mwenye kuhitaji.*"

Paulo alifanya kazi kwa mikono yake aakitengeneza mahema alipokuwa akisafiri ili kuweza kujisaidia mahitaji yake.

Mdo. 18:1-3, "*Baada ya mambo hayo, Paulo akatoka Athene akafika Korintho. Akamwona Myahudi mmoja, jina lake Akila mzaliwa wa Ponto, naye amekuja kutoka nchi ya Italia siku za karibu, pamoja na Prisila mkewe kwa sababu Klaudio amewaamuru Wayahudi wote watoke Rumi, naye akafikilia kwao; na kwa kuwa kazi yao ya ufundi ilikuwa moja akakaa kwao wakafanya kazi pamoja, kwa maana walikuwa mafundi wa kushona hema.*"

Mmoja hawezi kukaa pembeni na kuwaacha wengine wafanye kazi ambazo tunapaswa kufanya sote.

Msaada una manisha kusaidia au kusaidia katika kazi. Hivyo kwa tafsiri, mtu anatakiwa kufanya juhudi binafsi kabla mtu mwingine hajaamua kumsaidia. Kama yule mwingine anafanya kazi zote, huo sio msaada.

- Zab. 28:7, "*BWANA ni nguvu zangu na ngao yangu. Moyo wangu umemtumaini, nami nimesaidiwa; basi moyo wangu unashangilia, nitamshukuru.*"
- Zab. 31:23, "*Mpendeni BWANA, ninyi nyote mlio watauwa wake. BWANA huwahifadhi waaminifu, humlipa atendaye kiburi malipo tele.*"

Tunaweza tukawa na msaada mtakatifu kwa juhudi zetu za maombi

Rum. 8:26-27, "*Kadhalika Roho naye utusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe utuombea kwa kuugua kusikowezaa kutamkwa. Na yeye aichunguzaye mioyo aijua nia ya Roho ilivyo kwa kuwa huwaombea watakatifu kama apendavyo yeye.*"

Ni kama mtoto mdogo anayejaribu kuandika herufi kwa ugumu na mtu mzima anamsaidia.

Tunaweza kuwa na msaada mtakatifu tukianguka dhambini

1 Yoh. 2:1-2, "*Watoto wangu wadogo nawaandikia haya ili kwamba msitende dhambi. Na kama mtu aakitenddaa dhambi tunaye Mwombezi kwa Baba, Yesu Kristo mwenye haki, naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali kwa dhaambi za ulimwengu wote.*"

Mpatanishi – msaidizi. Anatusaidia kupigana na majaribu yetu.

Tunapaswa kujaribu tusitende dhambi, lakini ikitokea tukafanya yote haijapotea. Yesu yupo anatusaidia tukiziacha dhambi zetu na kuomba msamaha.

Simoni mchawi. Mdo. 8:9-24, "*Na mtu mmoja jina lake Simoni, hapo kwanza alikuwa akifanya uchawi katika mji ule, akiwashangaza watu wa taifa la Wasamaria, akisema ya kuwa yeye ni mtu mkubwa. Wote wakamsikiliza tangu mdogo hata mkubwa, wakisema,mtu huyu ni uweza wa Mungu ule Mkuu. Wakamsikiliza kwa maana amewashangaza muda mwingi kwa uchawi wake. Lakini walipomwamini Filipo akizihubiri habari njema zaa ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa wanaume na wanawake. Na yeye Simoni mwenyewe aliamini akabatizwa, akashikamana na Filipo; akashangaa alipoziona ishara na miujiza mikubwa inayotendeka. Na mitume walikuwako Yerusalemu waliposikia ya kwamba Samaria imelikubali neno la Mungu, wakawapeleka Petro na Yohana; ambao waliposhuka wakawaombea wampokee Roho Mtakatifu; kwa maana hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu. Hata Simoni alipoona ya kuwa watu wamepewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono ya mitume, akataka kuwapa fedha akisema, nipeni na mimi uwezo huu ili kila mtu nitakaye mweka mikono yangu apokee Roho Mtakatifu. Lakini Petro akamwambia fedha yako na ipotelee mbali pamoja nawe, kwa kuwa umedhani ya kuwa karama ya Mungu yapatikana kwa mali. Huna fungu wala huna sehemu katika jambo hili, kwa kuwa moyo wako si mnyofu mbele za Mungu. Basi tubia uovu wako huu ukamwombe Bwana, ili kama yamkini usamehewe fikira hii ya moyo wako. Kwa maana nakuona u katika uchungu kama nyongo na tena u katika kifungo cha uovu. Simoni akajibu akasema niombeeni ninyi kwa Bwana, yasinifikilie mambo haya mliyosema hata moja.*"

Pia tunawezaa kupata msaada wa ndugu zetu

Yakobo 5:16, "*Ungameni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana mpate kuponywa. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii.*"

Malaika wanasimama tayari kwa kutusaidia.

Heb. 1:13-14, "*Je! Yuko malaika aliyemwambia wakati wo wote, uketi mkono wangu wa kuume hata nitakapoweka adui zako chini ya nyayo zako?*"

Inafariji kujua kwamba kuna malaika wanawalinda watakatifu.

Hitimisho

Mungu, Kristo, neno la Mung, Roho Mtakatifu, na malaika wote wanawafikia watoto wa Mungu ili kuwasaidia wakati wa hitaji.

Hataivyo somo hili kimsingi imeelekezwa kwa Wakristo, ssitaasshindwa kuwaruhusu wenye dhambi waliopotea (wale ambao hawajafanyika Wakristo) kufahamu kwamba yeye pia anaweza kupata msaada kutoka upande mtakatifu.

- Rum. 5:6-8, "*Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia Kristo alikufa kwa ajili ya waovu. Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki; lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema. Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.*"
- 1 Yoh. 2:2, "*Naye ndiye kipatanisho kwa dhambi zetu; wala si kwa dhambi zetu tu, bali na kwa dhambi za ulimwengu.*"

Mtu anafanyikaje Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu zinazofanya hilo liwezekane:

. Imani. Waeb. 11:6, "Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu, umri sawa na wa kwangu alikuwa haamini kuwa Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye ana kwa ana kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ili kuwa ni nzuri. Lakini ili kuwa upande ambao ni salama, labda anaweza kwenda kanisani, na kama akifa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda kama Mungu akiona kuwa amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri na kwamba Mungu atamruhusu kuingia mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "mambo haya hayafanyi kazi kwa njia hiyo. Lazima umwamini yeye kwa moyo wako wote, la sivyo huwezi kumpendeza."

. Toba. Matend. 2:38, "*Petro akawambia, tubuni mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Matend. 11:18, "..... *Mungu amewapa pia mataifa toba liletalo uzima."* Kama ulikuwa una lala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani humu!" unachukuwa simu na taratibu unawapigia polisi, ukiwambia kwamba kuna mwizi ndani kwako, na unawapa anwani ya nyumba yako. Kidogo, unawasikia wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, "samahani; samahani!" anaomba msamaha wa nini? Anaomba msamaha kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena na anataka kubadilisha maisha yake ili kwamba asiibe tena. Ni badiliko la akili linalo leteleza badiliko la matendo. Hicho ndicho tunachotakiwa kukifanya kabla hatujawa Wakristo.

. Kukiri. Warumi 10:9-10*, "Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hatakupata haki, na kwa kinywa hukiri hatakupata wokovu."*

Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu. Kumbuka kwamba katika somo hilo hapo juu imani (kuamini), toba na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima, au wokovu. "Katika" humaanisha kuelekea kitu fulani; si kwamba mtu tayari ameshapata.

. Ubatizo. Ni katika ubatizo ndipo haki inapatikana, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa ili kuitimiza haki yote,

"*Lakini Yohana alitakakumzuia, akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa alipanda kutoka majini, na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa mpendwa wangu ninayependezwa naye*." (Math. 3:14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi ya kufanya. Unaona ni jinsi gani ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alipobatizwa? Yesu pia alisema "*imekuwa kwetu* ***sisi*** *kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yake yote, siyo kwa sababu ni haki yetu.

Hakika, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, tubuni makabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend. 2:38). Petro, ulisema ubatizo ni kwa ajili ya nini? *"Kwa ajili ya ondoleo la dhambi."* Kwa nini mtu mwingine anaacha hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

Yesu aliamuru kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. *"Akawaambia, enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu kama hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ukabatizwe uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana."* (Matend. 22:16).

Ubatizo ni agizo lililotolewa na Mungu.

Ubatizo unaitwa maziko. "*Hivyo mnazikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kama vile Kristo alivyofufuka katika wafu kwa utukufu wa Baba, hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale ni lazima ufe. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaungana kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."* (Rum. 6:3-6).

Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Kristo katika maisha yetu kwa njia ya ubatizo. Tunakuwa huru kutoka katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapobatizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hapo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatuendi makaburini na kuchukua udongo kidogo na kuweka juu ya mwili wa marehemu.

Kama hujafanyika mshiriki wa kanisa la Kristo, kwa nini usizingatie leo?